BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO ZILIZOWASILISHWA MEZANI NA SERIKALI KWA MWAKA 2021

February, 2022.

YALIYOMO

UTANGULIZI 2

1.0 Maelezo ya Utangulizi 2

1.2 Mamlaka ya Kutunga Sheria 2

1.3 Udhibiti wa Utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo 3

1.4 Namna ambavyo Kamati inatekeleza majukumu yake 5

2.0 UWASILISHWAJI MEZANI WA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA MWAKA 2021 6

2.1 Kufanya Uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote ambayo inatumika 6

3.0 UCHAMBUZI WA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO ZILIZOWASILISHWA 2021 8

A. Mgongano wa maneno ya pembeni na kanuni husika 17

(i) kanuni ya 24(1) Kanuni za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, 2018 18

(ii) Kanuni ya 40 ya Kanuni za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, 2018 18

B. MAREKEBISHO YA LUGHA 18

C. MAKOSA YA HERUFI 18

4.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA 19

5.0 HOJA 21

6.0 HITIMISHO 22

VIAMBATANISHO 24

UTANGULIZI

1.0 Maelezo ya Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo, nakushukuru kwa kutoa idhini kwa Kamati yangu iweze kuwasilisha **Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo** kuhusu Uchambuzi wa kanuni zilizowasilishwa Mezani na Serikali mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, natumaini kuwa ripoti hii itawezesha Waheshimiwa Wawakilishi kutoa ushauri zaidi kuhusu Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizochambuliwa na Kamati pamoja na Kanuni nyingine ambazo zinatumika. Pia, Kamati inaamini kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Wawakilishi ili kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati.

1.2 Mamlaka ya Kutunga Sheria

Mheshimiwa Spika, **Ibara ya 78 ya Katiba ya Zanzibar, 1984**, imeipa Baraza la Wawakilishi mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya yasiyo ya Muungano yahusuyo Zanzibar,

> "*Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi"*

Aidha, Ibara ya 78(2) ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

> *"Bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, nguvu za kutunga sheria katika Baraza la Wawakilishi itakuwa kwa kupitishwa Miswada katika*

Baraza la Wawakilishi."

Mheshimiwa Spika, pamoja na mamlaka hayo, Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa **Ibara ya 79(6) cha Katiba ya Zanzibar, 1984** limekasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali kutunga sheria Ndogo ndogo *(subsidiary legislation/delegated legislation)* ambazo hujumuisha Kanuni mbalimbali *(rules and regulations)* pamoja na Sheria Ndogo ndogo za Serikali za Mitaa *(By-Laws)* kama zinavyotafsiriwa chini ya **Sheria ya Tafsiri ya Sheria Nam. 7 ya Mwaka 1984**.

1.3 Udhibiti wa Utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hubaki katika mikono ya Baraza la Wawakilishi *(House Control Over Subsidiary Legislation.* Utaratibu huu ni wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola ambao unalenga kuliwezesha Baraza la Wawakilishi kujiridhisha juu ya matumizi ya mamlaka hayo ya kutunga sheria lililoyakasimu kwa mamlaka nyingine.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umezungumziwa na waandishi wengi wakiwemo Jain and Jain katika kitabu chao kiitwacho The *Principles of Administrative law* (2007) ukurasa wa 175 wanaposema;

Naomba kunuu kwa tafsiri isiyo rasmi;

> *".....kwa kuwa Baraza la Wawakilishi limetoa madaraka ya utungaji sheria kwa vyombo vingine, wajibu wake mkubwa ni kuhakikisha kunakuwepo matumizi sahihi ya madaraka yaliyo kasimiwa ya kutunga*

sheria, kusimamia na kudhibiti matumizi ya mamlaka hayo ili kuondoa uwezekano wa vyombo hivyo kutumia vibaya madaraka yaliyokasimiwa.." **Mwisho wa kunukuu**

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo utaratibu wa kuchambua Kanuni na kutoa Taarifa ndani ya Baraza kunaliwezesha Baraza la Wawakilishi kujiridhisha na namna madaraka yake yaliyo kasimiwa kwa Taasisi za Serikali yanavyotumika.

Mheshimiwa Spika, suala la udhibiti wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo pia limewekwa katika **Sheria ya Tafsiri ya Sheria,** ***(The Interpretation of Laws Act,)*** ambayo imeweka masharti maalum yanayolipa Baraza la Wawakilishi mamlaka ya udhibiti wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Hata hivyo udhibiti huo siyo wa moja kwa moja kwa sababu Baraza la Wawakilishi halina mamlaka ya kuingilia mchakato wa kutungwa kwa Kanuni yoyote mpaka Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo zinapotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na kuwasilishwa Barazani.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa kufanya Udhibiti wa Utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo, **Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020** ikisomwa kwa pamoja na Jadueli la kwanza la Kanuni hizi, imeanzisha majukumu ya Kamati hii kama ilivyo kwa Mabunge mengine katika Nchi za Jumuiya ya Madola. Miongoni mwa majukumu yake ni;

(a) kufuatailia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye repoti ya Kamati ya Mwaka;

(b) kuchambua Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa ya masharti ya Katiba, Sheria Mama na sheria nyengine;

(c) kujadili na kutoa mapendekezo kwa taasisi husika juu ya namna bora ya kutengeza kanuni na sheria ndogo ndogo;

(d) kulishauri Baraza kubatilisha Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ambazo zinakiuka masharti ya Katiba, masharti ya Sheria Mama au sheria nyenginezo za nchi;

(e) kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika

1.4 Namna ambavyo Kamati inatekeleza majukumu yake

Mheshimiwa Spika, wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, kama ambavyo imeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

Aidha, Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hutungwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Sheria Mama katika masuala mbalimbali. Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zinajumuisha:-

1. Amri *(Orders)*
2. Matamko *(Proclamations)*
3. Kanuni za Taasisi *(Rules)*
4. Kanuni za Mahakama *(Rules of Court)*
5. Kanuni za Wizara *(Regulations)*
6. Taarifa *(Notices)*

7. Kanuni na Sheria Ndogo ndogo za Halmashauri (*By – Laws)*
8. Hati *(Instruments)*

2.0 Uwasilishwaji Mezani wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo katika Mwaka 2021

Mheshimiwa Spika, Kanuni zetu za Baraza zimeweka sharti la kuletwa Barazani Kanuni au Sheria ndogondogo iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Baraza la Wawakilishi baada ya kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Baada ya Baraza la Wawakilishi kupokea Kanuni hizo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni na ushauri kuhusu yaliyomo katika Kanuni husika. Katika kutekeleza hayo Kanuni zetu za Baraza zimeainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa na Baraza la Wawakilishi. Hatua hizo ni:-

i) **Kutoa Azimio la kuzuia kutumika kwa Kanuni au Sheria Ndogo husika** ***(disallowance resolution)***

Kanuni inaruhusu Baraza la Wawakilishi kupitisha Azimio la kuzuia kutumika kwa Kanuni au Sheria Ndogo endapo litajiridhisha na maoni ya Kamati kwamba, Kanuni haikidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine ya nchi.

ii) **Kufanya marekebisho au kubadili Kanuni au Sheria Ndogo yoyote kufuatia Azimio la kuzuia kutumika kupitishwa na Baraza la Wawakilishi** ***(amendment and substitution)***

Katika kutekeleleza mamlaka yake yaliyoainishwa katika aya ya (i), Baraza la Wawakilishi linaweza kupitisha Azimio muda wowote ili kurekebisha au kubadili Kanuni au Sheria Ndogo yoyote iliyozuiwa kutumika.

2.1 Kufanya Uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote ambayo inatumika

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya utekelezaji mpana wa **Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la 2020**, Kamati inaweza kufanya uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote kwa kuzingatia vipaumbele inavyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuliwezesha Baraza lako tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali, naomba kubainisha mambo ambayo yanayozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo hayo ni:-

a) Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo husika inakiuka Katiba ya Zanzibar, 1984;

b) Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Kanuni na Sheria Ndogo hizo au Sheria nyingine yoyote;

c) Iwapo Kanuni au Sheria Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria *(drafting principles)*;

d) Iwapo Kanuni au Sheria Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

e) Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo inatekelezeka kwa urahisi kiuchumi na kijamii, na

f) Makosa ya uandishi na uchapaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha uchambuzi wake kwa kuzingatia masuala yaliyotajwa, Kamati hubaini hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufafanuzi katika maeneo ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zenye dosari. Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari

zilizobainishwa na Kamati. Kila Wizara inayoguswa na hoja zinazoibuliwa na Kamati, huwajibika kufika mbele ya Kamati na kutoa maelezo kuhusiana na Kanuni yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo napenda nilijulishe Baraza lako Tukufu kuwa Taarifa hii inahusisha uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2021

3.0 UCHAMBUZI WA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO ZILIZOWASILISHWA 2021

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021 Serikali iliwasilisha Mezani Kanuni na Sheria Ndogo ndogo Arubaini na Nane (48). Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo ziligawanyika katika mchanganuo ufuatao:-

a) Kanuni za Wizara (*Regulations*) – 40

b) Amri (*Orders*) – 2

c) Kanuni na Sheria Ndogo ndogo za Halmashauri (*By – Laws*) – 6

Mheshimiwa Spika, katika kutilia nguvu masharti ya Kanuni ya 25 ya Kanuni za Baraza la Wawakilshi ambayo imeelekeza kuwa majadiliano ndani ya Baraza yatafanyika kwa lugha ya Kiswahili, hivyo, Kanuni 34 ambazo ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kuwasilishwa bila ya muambatano wa Kanuni au Sheria ndogo iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili zilirejeshwa kwa Taasisi husika. Kwa minajili ya kuwasaidia wananchi ambao ndio watumiaji au walengwa wakuu wa Kanuni hizo, Kamati ilitoa agizo kwa Taasisi hizo kuandika upya Kanuni na Sheria ndogo hizo kwa lugha ya Kiswahili na kuziwasilisha tena

Barazani.

Mhe. Spika, Kanuni zilizorejeshwa ni kama ifuatavyo:-

1. The Oil and Gas (Local Content) Regulations, 2021
2. The Oil and Gas (Upstream) General Regulations, 2021
3. The Zanzibar Broadcasting Licensing Regulations, 2021
4. The Property Tax (Specification of the Property or Categories of Properties) Order, 2021
5. The Borrowing, Lending, Grant and Debt Management Regulations, 2021
6. The Tax Administration and Procedures (Virtual Fiscal Management System) Regulations, 2021
7. The Consumer Representatives Council Regulations, 2020
8. The License for the Forest Reserve Regulations, 2020
9. Plant Breeders' Rights Regulations, 2020
10. The Zanzibar Tourism (Amendment) Regulations, 2020
11. The Medical Practitioners and Dentist (Code of Conduct) Regulations, 2021
12. The Fair and Competition Tribunal Rules, 2021
13. The Fees and Levies (Amendment) Regulations, 2021
14. The Civil Status Registrations (Amendment) Regulations, 2021
15. The Stamp Duty (Replacement of Schedule) Order, 2021
16. Order for Increasing Pecuniary Jurisdiction in Civil Cases, 2021
17. The Maritime Transport (Fees and Charges) Regulations, 2020
18. The Zanzibar Industrial Court Rules, 2021
19. The Zanzibar Food, Drugs and Cosmetics (Pharmacovigilance) Regulations, 2019

20. The Zanzibar Food, Drugs and Cosmetics Goods Manufacturing Practice Enforcement Regulations, 2019
21. The Zanzibar Election Petition Rules, 2020
22. Sanitation and Hygine Standards
23. The Zanzibar Food, Drugs and Cosmetics (Control of Cosmetics) Regulations, 2019
24. The Maritime Transport (Fees and Charges) Regulations, 2020
25. The Civil Status Registration (Amendment) Regulations, 2021
26. Control of Medical Products and Herbal Drugs Promotion Regulations
27. The State University of Zanzibar Academic Regulations, 2021
28. Water Supply (licensing) Regulations, 2021
29. The approval fees regulation
30. The value added tax (amendement) regulation, 2020
31. The Zanzibar Food, Drugs and Cosmetics (recall, handling and disposal of unfit medicenes and cosmatics)
32. The Zanzibar Food, Drugs and Cosmetics (control of medical devices) regulations,2019
33. The petroleum(sampling ang testing regulation,2020)
34. Saving and credit cooperative societies regulation,2019

Aidha, kati ya Kanuni 34 zilizorejeshwa ni Kanuni 4 tu ndizo zilizoweza kufanyiwa tafasiri na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili na hatimae kuwasilishwa tena katika Kamati kwa ajili ya kupitiwa. Kanuni hizo ni;

1. Tafasiri ya Kanuni za Kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar

2. Tafasiri ya Kanuni za Ukaguzi wa Elimu, 2020
3. Kanuni za Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Majaribio ya Kitabibu), 2019
4. Kanuni za Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Majengo, Uingizaji na Usafirishaji nje ya Zanzibar wa Bidhaa za Dawa na Malighafi) 2019

Mheshimiwa Spika, Kanuni zilizochapishwa kwa lugha ya kiswahili na kuwasilishwa Barazani kwa mwaka 2021 ni kama ifuatavyo;

1. Kanuni za Utendaji kwa Wanaotoa Masaada wa Kisheria, Zanzibar, 2021
2. Kanuni za Hijja, 2019
3. Kanuni za Malipo ya Wakili na Vakili katika kusimamia kesi za Jinai, 2021
4. Kanuni za Kuweka Utaratibu wa Utoaji Huduma zinazotolewa na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, 2020
5. Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. 2014
6. Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. 2020
7. Kanuni za Manispaa ya Mjini
8. Kanuni ya Manispaa ya Magharib A
9. Kanuni ya Manispaa ya Magharib B
10. Kanuni za Baraza la Mji Mkoani
11. Kanuni za Baraza la Mji Chakechake
12. Kanuni za Baraza la Mji Wete
13. Kanuni za Usafirishaji wa Abiria kwa Pikipiki na Bajaji, 2019
14. Kanuni Kuu ya Uvuvi (Marekebisho), 2020

Mheshimwa Spika, Katika kupitia Kanuni zilizofanyiwa tafasiri utata wa kisheria uliibuka

katika maeneo mawili(2). Eneo la kwanza ni uwepo wa neno 'Tafsiri' katika jina refu (long Title), na eneo la pili ni kuchapishwa tena kwa Kanuni pamoja na kupewa namba ya tangazo la sheria (Legal notice number) tofauti huku ikibeba saini ya Waziri asiekuepo ofisini wakati wa kuchapishwa Gazeti hilo.

3.1 Gazeti Rasmi la Serikali

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Tafsiri ya Sheria (No.7 ya 1984) imeweka masharti ya utungwaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ikiwemo kuchapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Aidha **kifungu cha 36 cha Sheria** hiyo ya Tafsiri imeweka lazima ya kusainiwa kwa sheria Kanuni hizo na mtu ambae ana mamlaka kwa wakati huo.

> ..... and if the person on whom such power is conferred has been replaced wholly or in part by another person, the power conferred by this subsection upon the original person may be exercised by the replacing person concerning all matters or things within his jurisdiction as if he were the original person.....

Nukuu isiyo rasmi:

> ".....na ikiwa mtu ambaye amepewa mamlaka hayo yamebadilishwa na kuwekwa mtu mwingine, mamlaka hiyo iliyotolewa na kifungu kidogo hiki juu ya mtu wa asili inaweza kutekelezwa na mtu aliyechukua nafasi hiyo kwa namna ileile kama alivyokuwa nayo mtu wa asili....."

Kwa maelekezo hayo ya sheria ni dhahir kuwa ili Kanuni iweze kuchapishwa na kutumika ni

lazima iwe imewekwa saini na mtu ambae ana mamlaka kwa wakati huo.

Hata hivyo, Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi baada ya kufanya tafsiri ya Kanuni zao zilitangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na kupewa namba (Legal Notice Number) tofauti na ile namba ya awali ila kanuni hizo ziliendelea kubeba saini ya Waziri ambae kwasasa hayupo madarakani. Kanuni hizo ni;

1. Kanuni za Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Majaribio ya Kitabibu), 2019
2. Kanuni za Chakula, Dawa na Vipodozi (Udhibiti wa Majengo, Uingizaji na Usafirishaji nje ya Zanzibar wa Bidhaa za Dawa na Malighafi) 2019

Kwa maoni ya Kamati hii, Kanuni hizi zilipaswa kufuta Kanuni za mwanzo na kubeba saini ya Waziri mwenye mamlaka hayo kwa mujibu wa Sheria ya Tafsiri. Kwa muktadha huo tunaielekeza Serikali kufuata taratibu za utungaji wa Kanuni na Sheria ndogondogo kama ilivyoelekezwa katika **Sheria No. 7 ya mwaka 1984**.

3.2 Jina Refu la Sheria (long title)

Mheshimiwa Spika, jina refu la sheria ni jina rasmi linaloonekana kwenye kichwa cha sheria. Aidha, jina refu linabeba madhumuni ya Sheria na hutumiwa na mahakama kutafsiri vifungu vya sheria husika. Jina refu husaidia katika kuondoa utata na mkanganyiko na hutegemewa kama mwongozo wa kuamua upeo wa Sheria. Kwa muktadha huo, jina refu ni sehemu ya sheria husika, hivyo linatakiwa kuendana na maudhui ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati hii kutoa maagizo ya kuzitafasiri Kanuni kwa lugha ya Kiswahili, kumetokea mkanganyiko wa jina refu kwa baadhi ya Kanuni ambazo zimeenda kutafasiriwa. Mkanganyiko huo unapelekea kuondosha maudhui ya Kanuni ile na kwa upande mwengine imeondoa uhalali wa Kamati hii kuipitia. Mfano:

1. Tafasiri ya Kanuni za Kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar
2. Tafasiri ya Kanuni za Ukaguzi wa Elimu, 2020

Mheshimiwa Spika, neno **"Tafasiri ya**" sio sehemu ya jina la Kanuni hizo na wala halibebi maudhui ya Kanuni hizo, hivyo uwepo wake katika jina refu imeondosha maana halisi ya Kanuni iliyokusudiwa. Hata hivyo, baada ya majadiliano mapana na sekta husika imeonekana kuwa hakukuwa na lengo la kuandika Kanuni hizo kwa lugha ya kiswahili ila tu tafasiri hizo sio kanuni bali ni kwa madhumuni ya kukidhi matakwa ya Kamati. Kamati inajuliza maswala yafuatayo:

1. Je kama tafasiri hizo hazikulenga kuwa Kanuni, je kulikua na haja gani ya kuzichapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali na hatimae kuwekwa mezani?

2. Je Serikali inaona shida gani kuzipa uhalali wa kisheria Kanuni hizo zilizotafasiriwa kwa kufuta kanuni za kingereza na kuondosha neno 'tafasiri ya'

3. Je Serikali haifahamu ya kuwa kuleta mbele ya Kamati Tafasiri ya Kanuni ni kwenda kinyume na Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi?

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati inaielekeza Serikali kuzipa uhalali wa kisheria Kanuni hizo kwa kufuta maneno 'tafasiri ya' na kubakisha jina halisi la Kanuni husika.

3.3 Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kwenda kinyume na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, baadhi ya Kanuni zinakwenda kinyume na masharti yaliyowekwa na Sheria Mama au na Sheria Nyingine za Nchi. Kifungu cha 42 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinabainisha kwamba, Kanuni na Sheria Ndogo yoyote inapaswa kutokiuka masharti ya Sheria ya Baraza la Wawakilishi inayotoa mamlaka ya kutungwa kwake au Sheria nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, Kanuni zote ambazo zimeainisha viwango vya faini kwa makosa mbalimbali, zilibainika kuwa na dosari ya kwenda kinyume na Sheria nyingine za Nchi hususan Sheria namba 7 ya 1984. Uchambuzi umebaini kuwa **Kifungu cha 42(e) cha Sheria** hii imetaka faini zozote zitakazoainishwa katika Kanuni au sheria ndogo zisizidi zaidi ya **Shilingi za Kitanzania Elfu Saba (Tsh. 7,000) au kifungo kisichozidi miaka miwili (2)**. Mfano wa kanuni ni:

(i) **Kanuni ya 53(2) Kanuni za Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. 2014**

"……atalazimika kulipa faini isiyopungua Tsh. 1,000,000……."

(ii) **Kanuni ya 26(5) Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu Baraza la Manispaa ya Mjini, 2019**

"…….atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania Laki

Tano na isiyozidi Milioni Moja……."

(iii) **Kanuni ya 10(3) Kanuni za Ukaguzi wa Elimu, 2020**

"……..atalazimika kulipa faini isiyopunguwa laki mbili za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Laki Tano za Kitanzania"

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo takriban Kanuni zote tulizozifanyia kazi faini zake ni zaidi ya kiwango kilichoainishwa katika kifungu hicho, hivyo zinaweza kupingwa mbele ya Mahakama kuwa zinakiuka matakwa ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, tunaielekeza Serikali kufanya mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria hiyo ambayo kimsingi haiendani na wakati uliopo sasa na kuwa kipingamizi cha utekelezaji wa kanuni mbalimbali katika visiwa vyetu.

Aidha **Kanuni ya 39(2)** ya Kanuni za Huduma Zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2014 inasema "Afisa yoyote atakaekwenda kinyume na kifungu hiki atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake ikithibitika Afisa huyo atalazimika kulipa punguzo la leseni hiyo au kurejesha nyongeza kwa mkataji leseni". Kanuni hii imeeleza ndani yake kuwa kosa hili limeainishwa ndani ya **Sheria ya Utumishi wa Umma, 2011** na adhabu yake imeainishwa katika sheria hiyo. Hivyo kuainisha adhabu nyengine katika kanuni kwa kosa hilo ambalo Sheria limeshainisha kunakinzana na kifungu cha 42 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria ya 1984.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar, 2020, imekipa mamlaka Chuo hicho kulipa na kuajiri watumishi wake wakiwemo wakufunzi. Kanuni hiyo imetoa uwezo kwa Chuo kulipa mishahara kwa waajiriwa wake.

Kanuni hii inakinzana na **Kanuni ya 13 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014** ambayo imekataza ulipwaji wa mishahara mara mbili kwa mtumishi wa umma. Watumishi walioajiriwa na Taasisi hiyo chini ya kanuni ya Kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti Zanzibar ni watumishi wa umma.

Kamati inashauri kuwa Kanuni hizi zingefanyiwa marekebisho ili kuendana na matakwa ya miongozo ya NACTE pamoja na matakwa ya sheria zinazohusu utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa awali kuwa Kanuni au Sheria ndogondogo haziwezi kwenda kinyume na Sheria zilizotungwa na Baraza lako Tukufu. **Kanuni ya 2** ya Kanuni za Hijja, Kamati ilishauri kuwa neno **'Bodi'** ambalo katika uchambuzi lilionekana kuwa lilipewa maana tofauti na ile iliyoainishwa katika sheria hivyo Kamati iliagiza neno hili litafasiriwe kama lilivyo tafasiriwa katika Sheria ya Kamisheni ya Wakfu

Mheshimiwa Spika, **kanuni 4 na kanuni ya 9 za Kanuni za Chakula, Dawa na Vipodozi (Uthibiti wa Majaribio Ya Kitabibu) 2019** zimetaja Mkurugenzi Mtendaji, nafasi ambayo haikuainishwa katika Sheria mama wala kuanzishwa katika Kanuni hiyo. Nafasi za kiungozi katika taasisi huanzishwa kwa misingi ya Sheria hivyo tunashauri Serikali kuifanyia marekebisho **Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi No.2 ya 2006** ili kuendana na matakwa ya Wakala.

3.4 Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kuwa na Makosa ya Uandishi

Mheshimiwa Spika, Kanuni zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa mwaka 2021 zimekuwa na makosa mengi ya kiuandishi. Makosa hayo yanahusisha yafuatayo:

A. Mgongano wa maneno ya pembeni na kanuni husika

Mheshimiwa Spika, maneno ya pembeni yaani marginal notes ni mwangaza wa kifungu husika na humsaidia msomaji kujua nini kinakusudiwa katika kifungu kile. Inapotokea maneno hayo kwenda tofauti kimaudhui na kifungu kilichokusudiwa hupoteza muelekeo wa msomaji wa sheria au kanuni ile.

(i) kanuni ya 24(1) Kanuni za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, 2018

Maneno ya pembeni yanasomeka "Wakala Kumuonya Mtaka Huduma". Kanuni yenyewe inazungumzia uwasilishwaji wa maoni na mapendekezo ya Mtaka huduma katika kuboresha huduma za Wakala.

(ii) Kanuni ya 40 ya Kanuni za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, 2018

Maneno ya pembeni yanasomeka "Uwezo wa Bodi Kufanya Marekebisho". Kanuni yenyewe inazungumzia uwezo wa Waziri kutunga miongozo kwa utekelezaji mzuri wa Kanuni hizi.

B. Marekebisho ya lugha

Mheshimiwa Spika, moja ya taratibu za uandishi wa kisasa wa sheria yaani *legal mordern drafting* ni uchaguzi wa lugha nyepesi, sahihi na inayoeleweka. Baadhi ya Kanuni zilizowasilishwa kwenye Kamati zimekua na mkanganyiko wa lugha kiasi ambacho mwananchi ambae ni mtumiaji anakosa uelewa wa kinachokusudiwa katika kanuni hizo. Mfano itaonekana katika majadweli yaliyoambatanishwa na ripoti hii.

C. Makosa ya herufi

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida mara baada ya Wakala wa Uchapaji kuchapisha nakala za awali ni jukumu la ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuipitia Kanuni ile na kuondosha yale

makosa ya kiherufi (typos) na makosa mengine ya kimantiki na hatimae Wakala huchapisha kanuni zilizohaririwa. Hata hivyo, bila ya Kamati kupata jibu sahihi wakati wa uchambuzi wa kanuni mbalimbali, kanuni nyingi zilikuwa na makosa ya kiherufi kama ilivyoainishwa katika majadueli yaliyoambatanishwa na ripoti hii.

4.0 MAPENDEKEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Baraza la Wawakilishi madaraka ya kutunga Kanuni na Sheria Ndogo ndogo, kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Kanuni au Sheria Ndogo hizo.

Mheshimiwa Spika, kamati inashauri Serikali iongeza idadi ya Rasilimali watu katika Ofisi za Manispaa na Mabaraza ya Miji na hasa vitengo vinavyohusika na upitiaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ili kuhakikisha kuwa Taasisi hizo zinatumia mamlaka yake kisheria ya kutunga Kanuni na Sheria ndogo kwa mujibu wa **Sheria No 7 ya 2014**. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa heshima na madaraka ya waheshimiwa Madiwani kulindwa kisheria kama ambavyo waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge wanavyoheshimika. Baadhi ya watendaji katika taasisi hizo kwa makusudi au kwa kutokujua nafasi ya Mhesimiwa Diwani katika Baraza la Mji wameonekana kutokujali heshima na mamlaka ya waheshimiwa Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuishauri Serikali kuajiri watu wenye uweledi katika fani husika ili kurahisha na kuboresha kazi inayokusudiwa. Hii imejidhihirisha katika ziara

ya Kamati ilipotembelea Manispaa na Mabaraza ya Miji mbalimbali ambapo baadhi ya watendaji hususan wanasheria hawakua na uweledi unaohitajika katika kazi zao.

Aidha, tunaishauri Serikali kuongeza rasilimali watu katika kitengo cha Sheria ndogondogo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ili kupunguza makosa yanayojitokeza mara kwa mara katika Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yanarekebishwa kabla ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Mamlaka zilizopewa jukumu la kutunga Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zote zenye dosari. Baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo ziwasilishwe Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati imegundua kuwa Mahakama ya mwanzo iliyopo katika Manispaa ya Mjini kukosa miongozo ya kisheria katika kusikiliza kesi zinazohusiana na sheria za Manispaa. Hali hii hupelekea Hakimu kutoa hukumu tofauti na shauri lililopo mbele yake. Kwa upande mwengine, kumekua na mvutano wa mapato yanayotokana na faini kati ya Manispaa na Mfuko wa Mahakama. Aidha, kukosekana kwa Mahakama kwa baadhi ya Manispaa pamoja na miongozo ya kuendesha kesi hizo kunapelekea kutopatikana haki inayostahili kwa watu wanaokamatwa na Manispaa hizo. Hivyo,

tunashauri Wizara husika kukaa pamoja na Mahakama kuona ni jinsi gani kutaanzishwa kwa Mahakama hizo katika Manispaa zote na vipi zitafanya kazi na wapi fedha zinazotokana na faini ziweze kwenda.

Mheshimiwa spika, licha ya kuwa Kamati kwa kiasi kikubwa imejiridhisha kwamba Kanuni zimefuata taratibu za utungaji ingawaje kumejitokeza kwa baadhi ya Kanuni kukosekana ushirikishwaji wa Wadau walio wengi wakati wa utungaji wake jambo ambalo ni kasoro kubwa kwa Kanuni hizo hasa ukizingatia kwamba zinagusa maisha ya kila siku ya kila mmoja wetu. Hivyo tunazitaka taasisi zote kushirikisha wadau ipasavyo katika utungaji wa Kanuni na Sheria ndogondogo

5.0 HOJA

5.1 Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria

Kwamba, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zina dosari mbalimbali..

Hivyo Basi, Baraza la Wawakilishi linaazimia kwamba, Wizara ambazo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zake zimebainika kuwa na dosari katika Majedwali zifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari hizo.

5.2 Kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.

Kwamba, baadhi ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

Na Kwamba, kukinzana huko ni kwenda Kinyume na masharti ya Kifungu cha 42 cha

Sheria ya Tafsiri za Sheria kinachotoa sharti kwa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kutokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama.

Na Kwamba, kukinzana huko kunaifanya Kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango ilichokinzana.

Hivyo Basi, Baraza la Wawakilishi linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, kufanya marekebisho katika Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Baraza lako tukufu kwa kutupa nafasi sisi Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kuwasilishwa ripoti yetu katika Baraza lako tukufu. Ni matumaini yetu kuwa, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii na Kamati nyenginezo katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha tunaishukuru Afisi ya Katibu wa Baraza na wasaidizi wake kwa kuhakikisha kuwa uwepo wa Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo ni muhimu sana kwa kuwa kwa kiasi kikubwa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ndizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba nimshukuru **Mhe. Dr. Mwinyi Haji Talib** (Mwanasheria Mkuu) kwa kushirikiana na Afisi ya Baraza kuipa mafunzo Kamati. Mafunzo hayo yaliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati

na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. **Mhe. Jamal Kassim Ali** (MBM)– Waziri wa Nchi, Fedha na Mipango
2. **Mhe. Masoud Ali Mohammed** (MBM) – Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
3. **Mhe. Tabia Maulid Mwita** (MBM) – WAZIRI wa Habari,Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar
4. **Mhe. Simai Mohammed Said** (MBM) – Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar
5. **Mhe. Omar Said Shaban** (MBM) – Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizowasilishwa mwaka 2021 na hatimaye kufanikisha kazi hii. Wajumbe wa Kamati hii ni kama ifuatavyo;

1. Mhe. Mihayo Juma N'hunga – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Zawadi Amour Nassor- **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
4. Mhe. Hamza Hassan Juma
5. Mhe. Mohammed Ahmada Salum
6. Mhe, Juma Makungu Juma

7. Ndg. Karima Abdulwahab- Katibu

8. Ndg. Abdu Maulid Haji- Katibu

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Mihayo Juma N'hunga,
MWENYEKITI
KAMATI YA YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO
BARAZA LA WAWAKILISHI
22 Februwari, 2022

VIAMBATANISHO

Jadweli la kwanza

USHAURI WA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA UCHAMBUZI WA KANUNI ZA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI (USAJILI WA MAJENGO, UINGIZAJI NA USAFIRISHAJI NJE YA ZANZIBAR WA BIDHAA ZA DAWA NA MALIGHAFI) 2019

SEHEMU YA KWANZA

A. Marekebisho ya Kanuni ya 1 kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta neno “zitajuilikana” liliopo baina ya neno “hizi” na “kama” na kweka badala yake neno “zitajulikana”

B. Marekebisho ya Kanuni ya 3 (ufafanuzi)

a) Neno “waziri”

Kuuingiza neno “masuala” baina ya neno “na” na “afya”.

b) Neno “OTC” liwekwe maana halisi kwa kiswahili kwani ufupisho wa maneno ya kiengereza. Aidha marekebisho hayo yafanyike kila linapojitokeza neno hilo. Pia maneno “duka la dawa baridi” yapatiwe ufafanuzi.

SEHEMU YA PILI

A. Marekebisho ya Kanuni ya (6) kama ifuatavyo:

a) Maneno ya pembeni yanarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya “muda wa maombi wa maduka ya dawa baridi (OTCs)” yasomeke “muda wa maombi ya duka la dawa baridi”.

b) Aidha kila linapojitokeza neno “maduka” lisomeke “duka” kwani katka utaratibu wa uandishi wa sharia umoja ni wingi.

c) Kuhusu suala la muda wa maombi umewekwa mwezi novemba, Kamati inahitaji ufafanuzi busara (rationale behind) ya kuweka mwezi wa Novemba ni nini na kwa nini isiwe mwezi wowote, kwani inaweza kukosesha Serikali mapato na kupelekea kuchochea watu kufanya biashara kinyume na utatatibu.

1. Marekebisho ya Kanuni ya (9)(3) kama ifuatavyo:

a) kuhusu kanuni ya ada na tozo ni za mwaka gani Kamati inahitaji maelezo.

B. Marekebisho ya Kanuni ya (18) kama ifuatavyo:

1. Katika kakuni ndogo ya (4) inarekebishwa kama ifuatavyo:

i) aya ya (d) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo :

“jina halisi la kimataifa lisilo la kibiashara la dawa na kiwango chake kwa kila bidhaa”.

ii) aya ya (k) inarekebishwa kwa kufuta “mabano” na kuandika upya kama ifuatavyo:

“njia ya usafirishaji ikiwa bahari, anga au barabara”

SEHEMU YA TATU

C. Marekebisho ya Kanuni ya (22) (2) kama ifuatavyo:

a) Kufanyiwa ufafanuzi wa neno daktari ili kurahisisha uandishi na kumsaidia msomaji kwani kila atakapolikuta neno daktari itajumuisha madaktari wote waliokusudiwa katika kanuni hii

D. Marekebisho ya Kanuni ya (27) kama ifuatavyo:

a) Kufuta asilimia iliyoandikwa kwa tarakimu na kuwacha maneno, ili kupatikana uyakini endapo kutatokezea mgongano. Aidha, uandishi wa Sheria unatuelekeza matumizi zaidi ya maneno kuliko tarakimu.

E. Marekebisho ya Kanuni ya (28) kama ifuatavyo:

i) aya ya (c) kwa kufuta neno “biasahara” liliopo baina ya neno “ya” na “ielezwe” na kuweka badala yake neno “biashara”

ii) aya ya (d) kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo:

“jina asili la Kimataifa lisilo la kibiashara lielezwe wazi”.

SEHEMU YA NNE

F. Marekebisho ya Kanuni ya (33) (3) kama ifuatavyo:

a) Kanuni iweke wazi muda wa rufaa kwa waziri kwa aliyekuwa hakuridhika na uamuzi (aggrieved part) wa wakala. Kwa kawaida muda wa rufaa huwa ni siku 30 kutoka tarehe ya uamuzi.

G. Marekebisho ya Kanuni ya (35) na (36) viunganishwe na visomeke kama ifuatavyo:

“Mtu yeyote ambae atakwenda kinyume au atashindwa kufuata masharti ya Kanuni hizi au ambae moja kwa moja au vyenginevyo atamsaidia mtu mwengine kwenda kinyume na masharti ya Kanuni hizi atakuwa amefanya kosa na akipatikana na hatia chini ya Kanuni hizi atapewa adhabu zilizoainishwa katika Sheria”.

Marekebisho ya kanuni 37 kama ifuatavyo:

Kanuni zinazofutwa zielezwa za mwaka gani na namba ya tangazo la kisheria (LN) Jadweli la kwanza lisomeke “chini ya kifungu cha 16(2) na kanuni(5)(1)” kama inavyosomeka katika Kanuni halisi.

MAELEZO YA JUMLA

Kamati imebaini maeneo mengi ya Kanuni hii yapo katika mfumo hasi. Kamati inashauri uandishi wa Kanuni uwe katika mfumo chanya badala ya hasi ili kurahisisha uwelewa kwa msomaji (reader friendly). Aidha, uandishi wa kisasa wa Sheria (modal

drafting) ndivyo unavyoelekeza.

Naomba kuwasilisha

Jadweli la Pili

USHAURI WA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA UCHAMBUZI WA KANUNI ZA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ZA (UTHIBITI WA MAJARIBIO YA KITABIBU) 2019

SEHEMU YA KWANZA

I) MAREKEBISHO YA KANUNI KANUNI YA 3 (UFAFANUZI)

a) Neno “muombaji” maneno “muombaji ni” yaliowekwa mabano yatoke,

b) Neno “mkusanyiko”

a) Kufuta neno “ya” liliopo baina ya neno “dawa” na “uchunguzi” na kuweka badala yake neno “za”.

b) Aidha, wajumbe wanahitaji ufafanuzi katika Aya ya (a) ya ufafanuzi wa neno hilo.

SEHEMU YA PILI

1. Marekebisho ya Kanuni ya (5) inayohusu maombi ya kufanya majaribio ya kitabibu.

A. Katika kakuni ndogo ya (1) inarekebishwa kama ifuatavyo:

i) Katika aya ya (b):

a) Kwa kufuta maneno “kiambatanisho cha” yaliopo baina ya neno “katika” na “cha” na kuweka badala yake maneno “jadweli la”.

b) Nambari ya kanuni ilizofanyiwa rejea katika jadweli haziko sawa kwani inasomeka kwa sasa “kanuni ya 4(1)(b)” lakini usahihi ni kanuni ya (5)(1)(b). Aidha marekebisho hayo hayo hao yafanyike katika jadweli la pili, tatu na la nne.

ii) Katika aya ya (f):

a) kwa kufuta neno “tarifa” na kuweka badala yake neno “taarifa”.

iii) Katika aya ya (g):

a) kwa kufuta neno “zilivyoa-inishwa” na kuweka badala yake neno “zilivyoainishwa”.

B. Marekebisho ya Kanuni ya (5)(2) kama ifuatavyo:

a) kwa kufuta neno“uanothibitisha” liliopo mwishoni mwa mstari wa pili na kuweka badala yake neno “unaothibitisha”

C. Marekebisho ya Kanuni ya (6)(2) kama ifuatavyo:

a) kwa kufuta maneno “kwa kuzingatia” yaliopo mwanzoni mwa kanuni ndogo hiyo na na kuweka badala yake maneno “bila ya kujali”

D. Marekebisho ya Kanuni ya (6)(2)(i) ifutwe kuepusha matumizi mabaya ya Mamlaka.

E. Marekebisho ya Kanuni ya (7)(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno “kwa kuzingatia” na kuweka badala yake maneno “bila ya kujali”

F. Marekebisho ya Kanuni ya Kanuni ya (7)(3) ambayo inapatikana katika nakala ya kiengereza lakini imekosekana katika nakala ya Kiswahili hivyo iwekwe.

SEHEMU YA TATU

A. Marekebisho ya Kanuni ya 8(3)

i) Katika Aya ya(a)

a) (i) na (ii) neno “anuani” liliopo mwanzoni yasomeke “jina”

b) (vi) ifutwe na kuandikwa upya kama ifuatavyo

“jaribio la kitabibu linalohusiana na dawa husika zilizo katika jaribio la kitabibu la awamu ya utafiti”.

ii) Katika Aya ya (c)

a) Kwa kufuta neno “anuani” kwani ndani ya nakala ya kiengereza yanasomeka (contact information) hivyo kutafuta neno nzuri ili liendane na nakala hiyo

B. Marekebisho ya Kanuni ya 8(7) kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta maneno “la kitibabu” yaliopo mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

b) Kwa kufuta neno “mhusika” liliopo baina ya neno “ya” na “wa” na kuweka badala yake “muhusika”.

C. Marekebisho ya Kanuni 8(8) kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta maneno “uwasilishwaji huo” na kuweka badala yake neno “kuwasilishwa”

D. Marekebisho ya Kanuni 8(9) kama ifuatavyo:

a) kuhusu nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji hajaonekana kuanzishwa kwake katika Sheria na Kanuni, Kamati inahitaji ufafanuzi. Aidha suala hilo pia limejitokeza katika sehemu ya nne kanuni ya (9).

b) Kwa kufuta neno “muafaka” liliopo mwishoni mwa mstari wa kwanza na kuweka badala yake neno “sahihi”

SEHEMU YA NNE

1. Marekebisho ya Kanuni ya 14(1)(e) kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta maneno “na, au” yaliopo mwishoni mwa mstari wa pili na kuweka badala yake “au” kwani vyote haviwezi kuwekwa pamoja kwa kawaida “na” inaunganisha, “au” inatafautisha hivyo haziwezi kwenda sambamba katika uandishi hivyo tunashauri itumike moja katika hizo mbili.

2. Marekebisho Kanuni ya 15(1) kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta neno “zinazotumika” liliopo mwishoni mwa kanuni hiyo.

3. Marekebisho kanuni ya 16(1). Kamati inahitaji ufafanuzi wa Wizara.

Marekebisho kanuni ya 18(6) inarekebishwa kama ifuatavyo:

Kwa kufuta maneno “na, au” yaliopo baina ya neno “Mkuu” na “mfamasia” na kuweka badala yake neno “au”.

SEHEMU YA TANO

4. Marekebisho Kanuni ya 21(8) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta neno “ya” liliopo mstari wa pili baina ya “au” na “(5)” wa Kanuni hiyo.

5. Marekebisho Kanuni ya 25(1) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuingiza maneno “Sheria na” baina ya neno “ya” na “kanuni”

b) Kwa kufuta neno “(uteketezaji)” yaliopo baina ya neno “Kanuni” na “ya” na kuweka badala yake maneno “ya uteketezaji”.

6. Marekebisho Kanuni ya 26(4) kama ifuatavyo:

a) Maneno “ndani ya muda” yaliopo baina ya neno “anaweza” na “ulioneshwa” utajwe muda husika.

7. Marekebisho Kanuni ya 27(8)(2) kama ifuatavyo:

a) Kanuni ieleze sharti au masharti ambayo wakala itayatumia katika uwanzishaji wa bodi au kamati kwani Kanuni inahitaji kuweka bayana jambo lolote linalokusudiwa kuanzishwa au kutekelezwa.

8. Marekebisho Kanuni ya 29(2) kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta maneno “na, au” yaliopo baina ya neno “vibaya” na “uzembe” na kuweka badala yake neno “au”

9. Marekebisho Kanuni ya 29(3) kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta neno “inayotumika” liliopo baina ya neno “sheria” na “Zanzibar” na kuweka badala yake neno “za”.

10. Marekebisho Kanuni ya 30(5) kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta neno “watu” liliopo baina ya neno “mtu na “wanaofanya”. Pamoja na hayo marekebisho wajumbe wameona kuwepo kwa neno “Taasisi” badala ya watu kama itaonekana inafaa.

11. Katika marekebisho ya jadweli kama ifuatavyo:

a) Jadweli la sita kifungu husika kiwe kifungu cha 7(3) badala ya 6(3).

b) Jadweli la saba kifungu husika kiwe kifungu cha 32(3) badala ya 31(3).

Naomba kuwasilisha

Jadweli la Tatu

YALIYOBAINIKA NA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA UCHAMBUZI WA KANUNI ZA ZA HIJJA

UK	MAPUNGUFU	INAYOSOMEKA SASA	MAPENDEKEZO YA KAMATI
395	Sehemu ya Kwanza	kuchwa cha habari katika sehemu hii kinasomeka **UTANGULIZI**	Kufuta neno hilo na kuweka badala yake maneno **MASHARTI YA AWALI**
686	Kanuni ya 2	a) Maana ya neno "**Bodi"** b) Maana ya neno "Kamisheni" c) Maana ya neno "Kampuni" d) Maana ya neno "Sheria"	Neno hili lisomeke kama lilivyo katika Sheria ya Kamisheni ya Wakfu kwani limekwisha tafsiriwa Kufuta maneno mwishoni mwa maana ya neno hilo kama ifuatavyo "iliyoanzishwa na Sheria Namba 2/2007". Kufuta maneno "na marekebisho yake" yaliopo mwishoni mwa maana ya neno hilo. Kufuta maneno "pamoja na marekebisho yake" yaliopo mwishoni mwa maana ya neno hilo

396	Kanuni ya 3	*(a)* Katika aya ya **(a)**(i)	maneno i)"wasiopungua 50" yanahitaji ufafanuzi zaidi jee ni kwa muda gani. "50" iandikwe kwa maneno. Aidha marekebisho haya yafanyike kila yanapojitokeza namba katika Kanuni hii.
396	Kanuni ya 4	ngu cha kidogo cha 2 kama inavyosomeka katika rasimu ya Kanuni hii	inapendekeza Kanuni hii irekebishwe katia kifungu kidogo cha 2 kwa kukifuta na kukiandika upya vyo baada ya kupokea maombi ya kampuni na kuyafanyia kazi inaweza kuyakubali au kuayakataa kwa kuzingatia masharti ya kampuni ya kusafirisha mahujaji

	Kanuni 6	• Maneno "ili kujitetea……." Mpaka mwisho	Kamati inapendekeza kanuni hizi zirekebishwe kwa kufuta maneno hiyo mpaka mwisho wa kifungu kidogo hicho na kuweka badala yake maneno **"kueleza sababu za kutofutiwa kibali"** Aidha kamati inashauri **Muda wa kukata rufaa uainishwa.**

Jadweli la Nne

USHAURI WA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA UCHAMBUZI WA KANUNI ZA USAFIRISHAJI WA ABIRIA KWA PIKIPIKI NA BAJAJI

SEHEMU YA KWANZA

1. Marekebisho ya Kanuni ya 3 (UFAFANUZI)

a) Neno “Abiria” linarekebishwa kwa kufutwa na kuandika upya kama ifuatavyo:

“maana yake ni mtu aliyepakiwa katika pikipiki au bajaji ya usafiri wa biashara”

b) Neno “bajaji” kamati inashauri kuwepo ufafanuzi uwekwe vizuri zaidi kwa kuainisha uwezo wa mashine ya chombo husika.

c) Neno “chombo” lipatiwe ufafanuzi katika ufafanuzi wa maneno. Kwani katika kanuni hii limetumika sehemu nyingi kama katika Kanuni ya 4(2) (c)(f)(g)(h) ,13(1), 14(b)(c) (e), 15(f). Aidha, Kamati inashauri kufutwa kwa aya ya k, kwani Kanuni inahitaji kuweka bayana jambo lolote linalokusudiwa kuanzishwa au kutekelezwa.

SEHEMU YA PILI

2. Marekebisho ya Kanuni ya (5)(2) kama ifuatavyo:

a) kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

“bila ya kujali masharti ya kanuni ya kwanza ya kanuni hii mamlaka haitatoa lesini ya chombo kwa muombaji kwa:”.

b) kwa kufuta aya ya (e) kwani Kamati imebaini kwamba kanuni hiyo inaweza kutumika vibaya na kama mamlaka inaona kuwa kuna sababu ya msingi iweke wazi.

c) kwa kuongeza kanuni ndogo ya 5(3) kama ifuatavyo:

“iwapo maombi ya leseni ya biashara yatakataliwa mamlaka itamjulisha muombaji

pamoja na kueleza sababu za kukataliwa ombi lake".

3. Marekebisho ya Kakuni ya 6 kama ifuatavyo:

a) Kwa kufuta maneno "Pikipiki au Bajagi" yaliopo katika Kanuni hiyo kwani maneno hayo yamo katika tafsiri ya maneno"leseni ya chombo cha biashara". Aidha, marekebisho hayo yafanywe katika Kanuni ya 7.

4. Marekebisho ya Kakuni ya 9(3) katika Kanuni hiyo Kamati inashauri faini iliyokusudiwa iainishwe.

SEHEMU YA TATU

1. Marekebisho ya Kanuni ya 13 (1) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) Katika aya ya (h) kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"bajaji na pikipiki iwe na vioo vyakuwezesha kuona nyuma"

b) Katika aya ya (g) kufuta maneno "(chain box)" yaliopo baina ya neno "mnyororo" na "na"

c) Katika aya ya (i) kwa kufuta maneno "chombo chake kina" na kuweka badala yake maneno "pikipiki yake iwe na"

d) Marekebisho ya Kanuni ya 13(2) imeweka faini ya kiwango kisichopungua Kamati inashauri kuwepo kwa kiwango cha juu kisichozini kiwango fulani kwani kutasaidia kuondoa urasimu kwa baadhi ya watendaji wanaotoa uamuzi. Aidha marekebisho hayo yafanyike kila yanapojitokeza katika kanuni hii.

2. Marekebisho ya Kanuni ya 14(1) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) Katika aya ya (g) kwa kufuta neno "helment" liliopo mwishoni mwa aya hiyo.

b) Katika aya ya (x), Kamati inashauri ikutwe aya hiyo, kwani inaweza kutumika vibaya na kama mamlaka inaona kuwa kuna sababu ya msingi iweke wazi.

3. Marekebisho ya Kanuni ya 14(2) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) kwa kufuta neno “akipatina” liliopo baina ya neno “na” na “na” kuweka badala yake neno“akipatikana”.

4. Marekebisho ya Kanuni ya 15(1) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) Katika aya ya (h) kwa kufuta maneno “ya vyakula alivyokula”.

SEHEMU YA NNE

Marekebisho ya Kanuni ya 16(1) inarekebishwa kama ifuatavyo:

Kwa kufuta maneno “pikipiki au bajaji” yaliopo mwanzoni mwa mstari wa Kanuni hiyo, kwani maneno hayo yameainishwa vyema ndani ya ufafanuzi wa neno leseni ya biashara imeshajitosheleza.

a) Katika aya ya (a) kwa kufuta maneno “ambaye hana” na kuweka badala yake maneno “bila ya”.

b) Katika aya ya (d) kuandikwa vizuri kwa kuitenganisha aya ya (d) na Kanuni ndogo ya 2.

c) Aidha, Kamati inahitaji ufafanuzi katika Kanuni ndogo 2

Marekebisho ya Kanuni ya 17(2) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) Kufuta neno “isisimamishwe” na kuwekwa badala yake neno “isisimamishe”.

b) Katika Kanuni hiyo iwepo Kanuni ya kuwezesha dereva kukata rufaa iwapo hakuridhika na uamuzi wa Mamlaka.

SEHEMU YA SITA

Marekebisho ya Kanuni ya 24, Kamati inataka kufahamu ni busara gani iliyotumika

katika kuamuru pikipiki na bajaji zisichorwe wakati vyombo vyengine vya usafiri vinachorwa.

MAELEZO YA JUMLA

A) Adhabu ziwekewe kiwango cha juu na chini ili kuepusha kutumika vibaya na mamlaka husika.

B) Vituo vya chombo vielezwe vipo chini ya Serikali kuu au Serikali za mitaa.

C) Tafsiri ya neno chombo liwekwe katika ufafanuzi kwani limetumika mara nyingi na wakati mwengine kuna mgongano wa matumizi.

MAJADWELI

Para ya B. Maneno plate number kwanza yapo kwa kiengereza. Pia wanataka ufafanuzi ya namba ya usajili.

Para ya C. 1 kwa kuingiza maneno “na bajaji” baina ya neno “pikipiki” na “kinachokubalika”

Para ya C.1- 4 na 5 neno “chombo” limejitokeza tena. Hivyo Kamati inasisitiza kuwekewa tafsiri ya neno hilo.

Para ya C.1 -7 kwa kuingiza maneno “na bajaji” baina ya neno “pikipiki” na “iliyojazwa”

Para ya C. 2.1

a. kwa kufuta neno “anyeongeza” liliopo baina ya neno “Muombaji” na “muda” na kuweka badala yake neno “anayeongeza”

b. kwa kufuta neno “anatakiw” liliopo baina ya neno “muda” na “awasilishe” na

kuweka badala yake neno “anatakiwa”

Para ya C. 2.2

a. kwa kufuta neno “bishara” liliopo mwishoni mwashoni mwa para hiyo na kuweka badala yake neno “biashara”

Para ya C.3. 4

a. kwa kufuta neno “receipt No” na kuliweka katika lugha ya Kiswahili.

NAOMBA KUWASILISHA

Jadweli la Tano

MAONI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGONDOGO KANUNI ZA KMKM ZA UCHUNGUZI NA UKAMATAJI WA MAGENDO (MAREKEBISHO), 2020

(A) Maoni ya Jumla

1. Je ni wadau gani ambao mliwashirikisha katika utungaji wa Kanuni Mama?
2. Je mlipofanya marekebisho ya Kanuni hizi mliwashirikisha wadau?
3. Kanuni hii ilikuja katika Kamati na maoni mbalimbali yalitolewa na nyinyi mliyapokea, Je ni sababu zipi zilizopelekea kuacha baadhi ya yale yaliyokubaliwa, mfano kuingiza tafsiri ya neno 'Taasisi nyengine'?
4. Kanuni hii iliyowasilishwa imefanyiwa marekebisho kwa kanuni 22 ambayo ni zaidi ya asilimia 91%, kwa taratibu za uandishi Sheria ikifanyiwa marekebisho zaidi ya asilimia 50 inatakiwa kufutwa na kuandikwa upya. Je kwanini mlishindwa kuifuta Kanuni hii na kutunganyengine?

(B) Jaduweli la Marekebisho

UK	Kanuni	Kanuni ilivyosasa	Maoni ya Kamati
582	6(b)	……neno "hakina kupatiwa" katika…….	Kufutwa neno 'hakina' na badala yake lisomeke 'hakuna'
582	13(c)	……neno "askari" nakuweka badala yake……	Kutenganisha neno 'nakuweka' badala yake lisomeke 'na kuweka'
582	14	Kanuni hii imeengeza kanuni mpya ya 19(A). Maneno ya pembeni yanasomeka 'Msingi mkuu wauthibitisha kosa la magendo'	Kufuta neno 'wauthibitisha' na kuandika maneno 'wa kuthibitisha'

583	14	Aya (a) hadi (e) sentensi zote zimeanzia na herufi kubwa	Sentensi za aya hizi zianze kwaherufi ndogo kwa mujibu wa taratibu za uandishi
583	14 (d)	…….hairuhusiwi kuingizwaau kutolewa……..	Kutenganishwa kwa neno ‘kuingizwaau’ na lisomeke ‘kuingizwa au’
583	14(f)	……..kosa la magendokama ifuatavyo:	Kutenganisha neno ‘magendokama’ na lisomeke ‘magendo kama’
583	14(f)(i)	…….katika Chombo kuweza kukitambua chombo chombo husika;	Neno ‘Chombo’ baada ya neno ‘katika’ lianze kwa herufi ndogo. Neno ‘chombo’ baina ya maneno ‘kukitambua’ na ‘chombo’lifutwe. Hivyo isomeke ‘……katika chombo kuweza kukitambua chombo husika’
583	14(2)	……inatakiwa kuhaki-kisha kuwa……muda siopindukia siku 30……..	Kufuta neno ‘kuhaki-kisha’ na kuandika ‘kuhakikisha’ Aidha kufuta neno ‘usiopindukia’ na kuweka neno ‘usiozidi’ Kuandikwa kwa maneno ‘thelasini’ baada ya namba ‘30’ na namba ziwe katika mabano
583	15(a)	Katikakanuni ndogo ya (1)…….	Kutenganishwa kwa neno ‘Katikakanuni’

583	17	……inarekebishwa ifuatavyo:	Kuongeza neno ‘kama’ katikati ya maneno ‘inarekebishwa’ naneno ‘ifuatavyo’
583	17(b)	……..na kanuni na kanuni ndogo nyingine……	Kuondosha neno ‘na kanuni’ ili kuondosha kujirejea kwa maneno
584	19	Aya ya (a) mpaka (d) zimeanza kwa herufi kubwa	Aya zote hizo zianze kwa herufindogo kwa mujibu wa utaratibu wa uandishi
584	22(B)	…..chombo kinacho-weza kuharibika’	Kufutwa neno ‘kinacho-weza’ nabadala yake kiandikwe upya na kisomeke ‘kinachoweza’
585	22		Kapatiwa ufafanuzi wa kanuni hii

Jadweli la Sita

MAONI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGONDOGO
KANUNI KANUNI ZA UCHAGUZI, 2020

UK	KANUNI	INAVYOSOMEKA SASA	HOJA ZA KAMATI
407	Kifungu cha Sheria	Chini ya Kifungu cha 144(1)	Kuongezwa neno '(c)' na isomeke 'Chini ya Kifungu cha 144 (1)(c)' Hii ni kwa sababu Kifungu hiki ndicho kilichotoa mamlaka kwa Tume kutunga Kanuni hizi
407	1	'…..kusainiwa na Mwenyekiti na kuchapishwa katika'	Kuondoshwa neno 'kuchapishwa' na badala yake kuwekwe neno 'kutangazwa'.
408	2	"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar, 1984;	Kuongeza neno 'ya' baada ya neno Zanzibar ili isomeke kama ilivyo katika Katiba. ….. maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;
408	2	"Mtegemezi" ……..mtoto wa kuzaa wa Kike au wa	Neno 'Kike' lianze na herufi ndogo

		kiume……..	
410	4	…….kwa mujibu wa kifungu cha 8 cha Sheria.	Kifungu cha 8 cha Sheria hakijaorodhesha majukumu hayo ila nacho kimefanya rejea Sheria ya Afisi ya Uchaguzi. Hivyo ni vyema kukifanyia rejea kifungu hicho cha Sheria halisi au kuyaorodhesha majukumu hayo katika Kanuni
410	5	……kama ilivyoelekezwa katika Sheria.	Kufanyiwa rejea kifungu halisi kilichokusudiwa ili kurahisisha kwa wasomaji
411	6(3)	……kitambulisho cha Mpiga Kura.	Kuongeza maneno 'kwa mujibu wa Sheria' baada ya neno Kura. Hii ni kuweka msisitizo wa kisheria kwa kitambulisho cha kura kinachohusika
411	9(1)	Muda wa Uandikishaji	Kufuta neno 'Muda' katika marginal note na kuweka neno 'Wakati'

			ili kuendana na kifungu cha Sheria husika.
411	9(5)	……..la Kanuni hizi. Muda wa Uandikishaji.	Kufuta maneno 'Muda wa Uandikishaji' Ni marginal notes zimeingia kimakosa
413	12(5)	…….ndani ya saa (48) tokea……	Kuandika kwa maneno 'arubaini na nane' kabla ya neno (48)
413	13(4)	…..siku iliyotolewa ua huo……..	Kufuta neno 'ua' badala yake kuandika neno 'uamuzi'
414	16(1)	…….katika Jadweli Kanuni hizi……	Kuongeza neno 'la' baada ya neno Jadweli na Kanuni
414	16(3)	…….ndani ya siku ishirini na moja……	Hizi siku 21 zimetokea katika kifungu kipi cha Sheria
417	22(4)	…….ada ya kiwango kama……	Kufuta maneno 'ada ya' na kuongeza maneno 'maalumu cha ada' baada ya neno kiwango
418	26(1)(a)	…..kwa Pingamizi ya ombi la Uhamisho wa taarifa……	Neno pingamizi na uhamisho yawe kwa herufi ndogo. Kufuta neno 'ya' na kuweka neno 'la'
442	Fomu No 11	NATHIBITISHA kuwa	Kufuta maneno

		BW/BIBI_____	BW/BIBI na kuandika ‘Bw/Bi’

Jadweli la Saba

YALIYOBAINIKA NA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA UCHAMBUZI WA KANUNI KANUNI ZA HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2014

UK	MAPUNGUFU	INAYOSOMEKA SASA	MAPENDEKEZO YA KAMATI
686	Sehemu ya Kwanza	kuchwa cha habari katika sehemu hii kinasomeka **UTANGULIZI**	Kufuta neno hilo na kuweka badala yake maneno **MASHARTI YA AWALI**
686	Kanuni ya 2	*(a)* Maneno ya Pembeni Yamesahauliwa	kanuni hii maneno ya Pembeni yasomeke "**kusomwa".**
		(b) Maneno **"Kanuni Za Huduma Zinazotolewa Na Mamlaka Za Serikali Za"**	kanuni hii maneno hayo yasomeke "**Kanuni za Huduma Zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za……."**
686	Kanuni ya 3	*(b)* Katika aya ya **(a)**limekosekana neno "ya ".	narekebishwa kwa kuongeza neno **"ya"** baina na neno **'kanuni"** na namba ***"6"*** **.**
687	Kanuni ya 8	inarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 51	Kamati inapendekeza Kanuni hii irekebishwe kwa kuongeza maneno

			yafuatayo mwishoni mwa kanuni hii ambayo yatakayosomeka **"na kuzipanga upya kanuni zinazofuatakulinganana mtiririko wa nambari wa nambari wa kanuni hizi"**
687-688	Kanuni ya14,15,16,17,18,19,20	• Maneno **"kama ifuatavyo……;"** yaliyojitokeza mwishoni mwa kanuni hizo. • Vile vile, katika majadweli hayo ambayo yanasomeka jadweli la …… katika kichwa cha habari cha jadweli hilo	Kamati inapendekeza kanuni hizi zinarekebishwe kwa kufuta maneno **"kama ifuatavyo hadi mwisho wa kanuni hizo"** **kwa sababu maneno hayo yapo katika kila jadweli;"** Aidha kamati inashauri neno **"namba"** ambalo limejitokeza katika jadweli la tatu katika Kanuni Mama lifutwe, ili kuwe na uwiano wa jadweli hilo na nyengine

Makosa ya kimaana katika Kanunu Mama Huduma Zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

- Kanuni ya 27 ya Kanuni Mama, Kamati inahitaji ufafanuzi kuhusu maegesho mengi ya gari yapo chini ya udhibiti binafsi (mamlaka binafsi)

Jee ni sahihi ruhusa kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri au Manispaa.

- Kanuni ya 28 ya Kanuni mama bado kanuni hii haijafanyiwa merekebisho yoyote licha ya Wizara kushauriwa na Kamati kuwa hakitekelezeki,

Hivyo, Kamati inapendekeza iangalie upya Kanuni hio.

- Kanuni 39 cha Kanuni Mama iangaliwe upya ili kuondoa mkanganyiko baina ya Kanuni hii na Sheria ya Utumishi wa Umma kwani kosa lipo katika Sheria ya Utumishi wa Umma Adhabu ipo katika Kanuni.

- Kanuni 44 ya Kanuni Mama, iangaliwe upya kwani utekelezaji wa Kanuni hii ni mgumu hasa ukizingatia suala la uwekaji na ufugaji wa wanyama kwa wananchi wengi nje ya mji ni shughuli ya kawaida.

- Kanuni ya 53 ya Kanuni Mama inamlazimu mwananchi kulipa ada ya uhaulishaji ardhi katika Mamlaka mbili .

Kamati inapendekeza ada ya uhaulishaji ardhi ilipwe katika Mamlaka moja na baadae kugawanywa katika Mamlaka nyengine zinazohusika .

- Kanuni ya 62 na 63 ya Kanuni Mama zinazungumzia ukodishaji wa ardhi kwa ujenzi wa mnara na ada ya ujenzi wa mnara,

- Kiuhalisia ukodishwaji wa ardhi kwa ujenzi wa minara unaweza kufanywa na Serikali au Watu binafsi.

- Kamati inataka ufafanuzi katika mambo yafuatayo:

Malipo ya asilimia tano chini ya Kanuni ya 62(2) inawahusu wote

Malipo ya ada kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya ujenzi inawahusu pia Taasisi za Serikali

- Kanuni ya 67 ya Kanuni Mama ambayo inazungumzia kuweka kumbukumbu za usafiri baharini iangaliwe vizuri kama haina mgongano na Mamlaka ya Usafiri Baharini.

- Kanuni ya 68(1) ya Kanuni Mama irekebishwe kwa kufuta neno **"imekidhi"** na kuweka badala yake neno **"limekidhi"** baina ya neno **"lake"** na "**vigezo"**

- Kanuni ya 76(d) ya Kanuni mama, Kamati imebaini kutoeleweka dhana ya Kanuni hiyo, hivyo basi inahitaji ufafanuzi.

- Kanuni imeainisha makosa na adhabu katika vifungu mbali mbali hata hivyo, Kamati imebaini kuwa hakuna uwiano wa adhabu hizo kati ya faini na kifungo, hivyo basi, Kamati inahitaji kupatiwa ufafanuzi juu ya vigezo vinavyotumika kuamua muda wa kifungo na faini.

- Kanuni hizi kwa kiasi kikubwa zimezungumzia utozaji wa tozo na ada katika vyanzo mbali mbali ada na tozo ambazo zilikuwa zikitonzwa na Mamlaka au Taasisi nyengine , Kamati inataka ufafanuzi kwa kiasi gani Taasisi zimeshirikishwa katika utungaji wa kanuni hizi.

- Jee utozaji huo wa ada na tozo hautufanya ulipaji wa malipo hayo mara mbili.